

HALMASHAURI YA WILAYA MASASI

(Barua zote zielekezwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)

Simu: 023 - 2510031.
Fax: 023 - 2510031
E-mail: ded@masasi.go.tz
Website: www.masasidc.go.tz



S.L.P. 60,
Masasi,
Mtwara,
TANZANIA.

Unapojibu tafadhali taja;

Kumb. Na. MDC/L.10/2/VOL.X/2

Tarehe: 16. 08. 2020

YAH: TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi anapenda kuwatangazia Watanzania wote wenye sifa zilizo rodheshwa kwenye tangazo hili nafasi moja (1) ya Ajira ya kudumu ya **Mtendaji wa Kijiji Daraja la III**. Ajira hiyo imetokana na kibali cha **AJIRA MBADALA** kutoka kwa Katibu Mkuu ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala bora, chenye Kumb. Na. FA 170/362/01 "A"/30 cha tarehe 13.07.2020.

1: MTENDAJI KIJIKI DARAJA LA III (NAFASI 1)

1.1: KAZI NA MAJUKUMU YA MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III

- Atakuwa Mtendaji na mshauri Mkuu wa Serikali na kamati zake katika kupanga mipango ya maendeleo na utekelezaji wa mipango.
- Atakuwa Afisa Mhasibu wa serikali ya Kijiji na atasimamia mapato na matumizi ya serikali ya Kijiji.
- Atakuwa mlinzi wa Amani na msimamizi wa utawala bora katika Kijiji
- Ataratibu na kusimamia upangaji na utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya Kijiji.
- Atakuwa Katibu wa serikali ya Kijiji
- Atatafsiri sera, taratibu na kusimamia utekelezaji wa sheria Ndogo za Kijiji
- Ataratibu na kuandaa taarifa ya utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuziwasilisha kwenye Halmashauri ya Kijiji na baada kwenye Mkutano Mkuu wa Kijiji na Kata.

- Ataratibu vikao vya maendeleo ya Kijiji vitakavyowahusisha wananchi na wataalam waliopo kwenye eneo lake.
- Atasaidia katika mikakati mbalimbali ya kuondoa njaa, umasikini na kuongeza uzalishaji mali
- Atasimamia na kuratibu matumizi bora ya nguvu kazi
- Atakuwa kiongozi wa wakuu wa vitengo vya kitaalam katika Kijiji
- Atasimamia ukusanyaji wa kumbukumbu za walipa kodi, wataalam mbalimbali na NGOs zilizopo katika Kijiji

1.2: SIFA ZA MWOMBAJI.

Awe amehitimu elimu ya kidato cha nne au cha sita na mafunzo ya Astashahada /Cheti katika moja ya fani zifutazo:- Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Jamii kutoka chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

1.3: Mshahara kwa kuzingatia Ngazi ya Mishahara ya Serikali **TGS B₁** kwa mwezi.


1.4: MASHARTI YA JUMLA

1. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania wenye umri kuanzia miaka 18 hadi 45
2. Waombaji wote waambatanishe cheti cha kuzaliwa.
3. Waombaji waambatanishe maelezo binafsi (CV) yenye anuani na namba zao za simu na majina mawili ya wadhamini.
4. Maombi yaambatanishwe na nakala za vyeti vya taaluma na kuhitimu mafunzo ya vyuo.
5. Maombi yaambatanishwe picha mbili "Passport size" ya hivi karibuni iandikwe jina kwa nyuma.
6. Waombaji waliosoma nje ya nchi waambatanishe cheti cha ulinganifu (equivalent certificate) kutoka Baraza la Mitihani Tanzania (NECTA) au kwenye Mamlaka.

7. Waombaji wenye vyeti vya ngazi ya NTA Level 4 'Basic Technician Certificate' (NTA level 4) maombi yao hayatafanyiwa kazi. Cheti kinachopokelewa ni 'Technician certificate' (NTA Level 5) na kuendelea.
8. Watakoachaguliwa kufanya usaili watajulishwa tarehe ya usaili kupitia tovuti ya Halmashauri www.masasidc.go.tz
9. Maombi yatapokelewa kuwanzia tarehe **17.08.2020** hadi tarehe **24. 08. 2020** kwa njia ya Posta
- 10: Maombi yatumwe Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Masasi kwa anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya,
S. L. P. 60,
MASASI.

WAOMBAJI WOTE MNAKARIBISHWA.



Changwa M. Mkwazu
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
MASASI